www.xtrapapers.com

Cambridge Assessment International Education

# Cambridge IGCSE™

**SWAHILI** **0262/02**

Paper 2 Listening **May/June 2021**

TRANSCRIPT **Approximately 45 minutes**

This document has **8** pages.

© UCLES 2021

www.xtrapapers.com



ENG: Cambridge Assessment International Education
Cambridge IGCSE Specimen Examination in Swahili
Paper 2 Listening, May/June 2021
Turn over now

*(Pause 5 seconds.)*

TLR: **Zoezi 1**

TLR: Utasikia vipande vinane vifupi vilivyorekodiwa.
Jibu swali 1–8 katika nafasi uliyopewa.
Majibu yako yawe mafupi iwezekanavyo.
Utasikia kila rekodi mara mbili.

TLR: Swali 1

M: * Habari gani Asha? Eti vipi maisha hapa, unapenda kuishi mjini Dodoma?

F: Ninapapenda sana. Nina marafiki wengi sana na maisha yangu yapo hapa sasa. Utotoni niliishi kule Malindi, karibu na ufukwe wa bahari.

M: Basi maisha yako yalikuwa tofauti kabisa!

F: Ndiyo, kwa kiasi fulani. Lakini sasa Dodoma ndiyo nyumbani, nimeshapazoea. Hata sijui itakuwaje ikibidi kuhama.

M: Utazoea tu!

F: Hapana, sidhani kama nitaweza. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 2

M: * Shikamoo Bi Mariamu, karibu sana hapa kwetu.

F: Marahaba; asante mwanangu.

M: Sasa, mimi nina swali moja tu, hivi wewe hupendelea zaidi kuimba katika lugha gani?

F: Unajua, ingawa nyimbo nyingi tulizorithi kutoka kwa mababu zetu ni za Kiarabu, na Kiingereza ni mashuhuri siku hizi, mimi binafsi huimba kwa Kiswahili kwani hii ni lugha inayopendeza kimuziki zaidi.

M: Alaa, kumbe! **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

www.xtrapapers.com



TLR: Swali 3

M: * Tangu utotoni nimekuwa na ndoto ya kujiajiri mwenyewe. Nilivutiwa sana na biashara za rejareja ingawa pale mwanzoni sikuwa na mtaji wa kutosha kuweza kuzifanya. Kutimiza ndoto yangu nilianza kwa kufanya kazi ya kubeba mizigo ya watu sokoni. Hii ilinichosha sana kwa sababu ya masaa marefu ya kazi. Hata hivyo, nimeweza kuwekeza pesa na sasa nina sehemu yangu mwenyewe hapa sokoni ambapo ninauza mboga. Ipo siku nitakuwa na duka langu mwenyewe. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 4

F: * Baada ya kusherehekea harusi iliyokuwa na waalikwa wengi mjini Lushoto, tulifika mji wa Arusha na kukuta hoteli zote zimejaa. Kwa bahati tu tuligundua nyumba ya mtu binafsi ambaye hupangisha vyumba kwa wasafiri. Kila chumba kilikuwa na pangaboi, meza na vitanda vinne. Vyoo vyote vilikuwa nje. Ilibidi kulala hapo. Safari yangu hiyo imenifunza jambo muhimu; sitaenda tena Arusha ikiwa kuna mkutano wa wakuu wa nchi za Afrika ya Mashariki. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 5

M: * Mimi ninaitwa Baraka. Juzi, timu yangu ya mpira ilifungwa moja bila, na wenzangu walinikasirikia sana. Wao wanahisi mimi ni mvivu na wanataka nikimbie kwa kasi zaidi uwanjani. Lakini, ukweli ni kwamba ningalikuwa na tatizo moja, basi lingekuwa ni hasira yangu. Kwa mfano, katika mechi moja, nilitolewa nje baada ya kumsukuma mchezaji mmoja aliyenitukana. Itabidi nijitahidi kupunguza hasira zangu za haraka haraka. Zitaniharibia maisha. Ninadhani nitaweza kwani zamani sikuwa hivyo. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 6

F: * Je, unafahamu sanaa ya ususi? Sasa unaweza kujifunza ujuzi huu ikiwa miongoni mwa wengine huku mkistarehe ndani ya afisi zetu. Utaweza kusuka mikoba, mikeka na makawa yenye nakshi na mapambo ya kuvutia. Kwa miaka mingi wengi wamefikiri kwamba wajibu mkuu wa ususi ni kutoa ajira, hasa kwa wanawake. Sasa, imegundulika kwamba ususi ni sanaa inayosaidia kupunguza msongamano wa mawazo. Karibuni nyote kila jumamosi kuanzia saa moja hadi saa tatu usiku. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 7

M: * Je Sia, ungependa kufanya kazi ya ualimu kama wazazi wako ukubwani?

F: Bila shaka, kazi hiyo ni muhimu. Lakini ninavutiwa na sheria. Ninathamini sana haki za binadamu na ninaamini binadamu wote wana usawa.

M: Ah basi lazima utakuwa wakili. Ni kazi nzuri na ina mshahara mzuri.

www.xtrapapers.com



F: Kwangu mimi pesa si muhimu sana, lakini hata hivyo kazi hiyo ndiyo ndoto yangu, kwa sababu ningependa kulinda haki za watu wote.

M: Vizuri sana! Kila la heri. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 8

F: * Habari zenu? Jina langu ni Alia. Nchini kwetu, maji ya bomba si masafi na huwa na vijidudu vinavyoweza kuleta magonjwa ya tumbo. Watu huchemsha maji ili kuviua. Nyumbani kwetu mama huchemsha maji ya kunywa na zaidi ya hapo mimi huyachuja katika madumu. Majirani zetu wanajiweza na wao hununua maji ya chupa. Sisi kwetu hatununui maji ya chupa kwani ni ghali sana na plastiki inaharibu mazingira yetu. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 1. Baada ya muda mfupi utasikia Zoezi 2. Tumia muda huu kusoma maswali ya Zoezi 2.

*(Pause 30 seconds.)*

TLR: **Zoezi 2**

TLR: Utamsikia msichana anazungumza kuhusu Reli za Kisasa.
Msikilize na malizia sentensi.
Andika neno moja au maneno mawili tu katika kila nafasi.
Utasikia rekodi mara mbili.

F: * Hivi karibuni nimegundua kwamba mifumo ya reli barani Afrika haijaungana. Kwa hivyo si rahisi kusafiri kwa reli kutoka nchi moja hadi nyingine. Kwa mfano, mtu hawezi kutoka Kenya, akavuka Tanzania na kufika Rwanda kwani kila nchi ina reli zake na reli hizi hazivuki mipaka ya nchi husika. Kuna umuhimu kwa reli hizi kuungana ili kuwezesha biashara, ushirikiano na pia jamii kuweza kuwa na mawasiliano ya karibu zaidi.

F: Jambo hilo limeanza kushughulikiwa kwani katika Afrika ya mashariki kuna nchi ambazo zimeanza kujenga reli za kisasa, mfano mmoja ni Ethiopia. Reli ya Ethiopia ni ya kisasa na inaunganisha Ethiopia na Djibouti. Pia ina stesheni 21 ingawa si zote zinazoweza kutoa huduma kwa wasafiri na mizigo. Ni stesheni 13 tu zenye uwezo wa kuwashughulikia wasafiri na mizigo pia.

F: Mimi si mgeni wa reli za kisasa kwani nimewahi kusafiri kwa kutumia reli ya kisasa inayounganisha Nairobi na Mombasa. Ni safari iliyonifurahisha sana kwani niliweza kutembelea chumba cha madereva na kukutana nao. Wote walikuwa wanawake wenye umri mdogo na wote walikuwa wamevaa sare nyekundu. Walipendeza sana.

F: Jina la treni ya kwanza ya kisasa iliyotoka Nairobi kuenda Mombasa ni Madaraka. Treni hiyo imeleta maendeleo mengi. Kwanza gharama za kuisafirisha imeshuka kwani safari ya treni ni bei ya chini kuliko ndege. Pia muda wa kusafirisha ni mchache kwani safari nzima huchukua saa tano tu. Usumbufu pekee ninaouona ni kwamba, stesheni za reli hizi zipo nje ya mji na si katikati.

F: Hivi sasa Tanzania ipo mbioni kumalizia ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza. Nina hamu ya kusafiri kati ya miji hiyo kwani bila shaka wasafiri wataweza kuona mengi huko ikiwa ni pamoja na nyika, milima na pia mabonde. Nimesikia kwamba ni wasafiri wachache

www.xtrapapers.com



watakaotumia huduma hii. Kwa hivyo, serikali haijafanya uamuzi kamili kuhusu idadi za safari za kila siku. **

*(Pause 30 seconds.)*

TLR: Sasa sikiliza tena.

*(Pause 3 seconds. Repeat from * to **. Pause 30 seconds.)*

TLR: Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 2. Baada ya muda mfupi utasikia Zoezi 3. Tumia muda huu kusoma maswali ya Zoezi 3.

(Pause 30 seconds.)

TLR: **Zoezi 3**

TLR: Utawasikia watu sita wakizungumza kuhusu matumizi ya plastiki Afrika ya Mashariki.

Oanisha wasemaji na mawazo katika orodha A–G. Kwa kila msemaji, andika herufi (A–G) katika mstari wa jibu.

Tumia kila herufi mara moja tu. Kuna herufi ya ziada isiyohitajika.

Utasikia rekodi mara mbili.

TLR: * Msimulizi 1

M: Mara ya kwanza niliposikia kwamba mifuko ya plastiki kwa ajili ya kubebea bidhaa itapigwa marufuku nilishangaa sana. Pia nilishtuka kuona picha za uchafu unaoletwa na watu kutupa mifuko, na nimehuzunika kusikia kwamba mifuko hiyo ni chanzo kikubwa cha wanyama wengi kupoteza maisha. Lakini, sijui sasa tutatumia mifuko gani ambayo itakuwa na nguvu kama hii ya plastiki. Nahisi ingekuwa bora kama serikali ingeruhusu matumizi ya mifuko ya plastiki lakini watu wainunue na hivyo kuwa na uchungu nayo na kutoitupa hovyo.

TLR: Msimulizi 2

F: Kupigwa marufuku kwa matumizi ya mifuko ya plastiki ni hatua nzuri ambayo serikali imechukua. Lakini tatizo si mifuko tu, tatizo ni bidhaa nyingi zinazotokana na plastiki kama chupa. Mimi huumia sana kuona ndege na ng'ombe wanapoteza maisha yao baada ya kula chupa za plastiki. Juzi kulikuwa na habari kuhusu yule kasa ambaye aliumizwa kwa mirija kukwama puani mwake. Uchafu wa plastiki ni tatizo kubwa ulimwenguni kwetu. Lazima kuwe na mbadala wa plastiki.

TLR: Msimulizi 3

M: Nimefarajika kusikia habari za Tanzania kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki. Sisi huku Kenya tulishapiga marufuku tangu zamani na sasa ni kawaida tu. Tunabeba bidhaa zetu za sokoni kwenye mifuko mbadala. Juzi nilinunua chapati zilizofungwa kwenye majani ya migomba. Zamani ningaliona jambo hilo ni kichekesho, lakini sasa nimeelewa kwamba kuna uchafuzi wa mazingira unaotokana na kutupa takataka kama plastiki hovyo. Na hizi huathiri mabadiliko ya tabia ya hali ya hewa duniani. Ni bora nusu shari kuliko shari kamili.

© UCLES 2021 

www.xtrapapers.com



TLR: Msimulizi 4

F: Juzi nilisoma kuhusu dau lililotengenezwa kwa matofali ya plastiki na kusafiri baharini bila ya tatizo lolote. Pia nimeona bidhaa zinazotengenezwa kutokana na chupa za plastiki ikiwa ni pamoja na viti na vigoda. Sasa nimeamua kufanya biashara kwa kutumia bidhaa za plastiki. Nitaanza kwa kutengeneza matofali ya plastiki ambayo nitayatengeneza kwa kujaza mifuko ya plastiki ndani ya chupa na kuziuza. Huu ndiyo utakuwa mchango wangu katika mapambano haya ya uchafuzi wa mazingira.

TLR: Msimulizi 5

M: Nimelisikia sana hili suala la uchafuzi wa mazingira kutokana na plastiki. Pia kuna mashirika na wajasiriamali wakitengeneza bidhaa tofauti na kujiendeleza kiuchumi kutokana na bidhaa za plastiki. Kuna fanicha, vifaa vya ujenzi na kadhalika. Lakini sasa kila mtu amekuwa balozi wa uchafuzi wa mazingira. Na serikali inapiga marufuku mifuko ya plastiki. Huu ni usumbufu tu kwa wananchi. Kwa mfano, mimi kamwe situpi takataka hovyo kwa hivyo nina uhakika takataka zangu haziwezi kufika mbali na kuathiri viumbe.

TLR: Msimulizi 6

F: Kuna watu wenye ubinafsi mkubwa ambao wanadai eti wao hawatupi taka hovyo kwa hivyo hawachafui mazingira. Hiyo si kweli! Halafu husema eti wangependelea hata kulipia mifuko ya plastiki ili waendelee kuitumia. Kosa lililoje! Unapotumia mfuko, unafahamu mfuko huo utaishia wapi? Hapana! Mfuko wa plastiki uliotupwa unahitaji miaka mingi ili uvunjikevunjike na kuwa uchafu ardhini. Kwa kweli tukifanya mchezo tutapoteza dunia yetu. Ni wajibu wetu sote kutunza mazingira na kuhakikisha kwamba tunabadilisha mienendo yetu. **

*(Pause 5 seconds.)*

TLR: Sasa sikiliza tena.

*(Repeat from * to **. Pause 30 seconds.)*

TLR: Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 3. Baada ya muda mfupi utasikia Zoezi 4. Tumia muda huu kusoma maswali ya Zoezi 4.

*(Pause 30 seconds.)*

www.xtrapapers.com



TLR: **Zoezi 4**

TLR: Utasikia mazungumzo kati ya Hannah na Steve.

Sikiliza mazungumzo hayo na soma maswali.

Kwa kila swali chagua jibu sahihi kati ya A, B au C.

Weka alama ya tiki kwenye kisanduku sahihi.

Utasikia rekodi mara mbili.

F: * Habari za asubuhi, Steve. Vipi nyumbani wote hawajambo? Nakuona kama una haraka leo?

M: Nzuri tu. Wote wazima. Leo nimetoa ahadi ya kuwapeleka wajukuu wangu wadogo sinema. Wana hamu kubwa ya kuiona filamu mpya iliyotoka. Ni filamu ya watoto isiyonivutia lakini ninataka kuwafurahisha. Itabidi niwafuate baada ya dakika chache.

F: Vizuri sana. Watafurahi bila shaka.

M: Ndiyo. Ingawa mimi nilipokuwa mtoto hamu yangu kubwa ilikuwa kusikiliza redio ya babu yangu nyakati za jioni. Kulikuwa na kipindi cha hadithi kilichokuwa na masimulizi ya kuvutia sana. Mtangazaji alisimulia hadithi pole pole.

F: Kweli? Mimi nilipokuwa mtoto nilipenda vipindi vya televisheni vya watoto lakini sidhani kama nilivisubiria hasa.

M: Hiyo ndiyo tofauti ya utoto wetu na ule wa nyakati hizi. Sisi tulikuwa hatuna haraka. Tuliamini kabisa umuhimu wa subira na kusema haraka haraka haina baraka. Ninasema hivyo kwani mara nyingi hadithi moja ilihadithiwa kwa wiki tatu au nne. Basi kila jioni, tulitulia kimya tukisikiliza maendeleo ya hadithi huku kila mmoja wetu akitumia mawazo na ubunifu wake binafsi kuelewa hadithi hizo na kujijengea picha ya kile alichosikia. Kila mtu alikuwa na picha tofauti za wahusika, nguo zao, nyumba walizoishi, mitaa yao.

F: Kweli inahitaji ubunifu kujenga picha ya masimulizi unayoyasikia. Mlikuwa mnahadithiwa hadithi gani?

M: Hadithi zilikuwa nyingi sana. Kulikuwa na hadithi za makabila tofauti kutoka duniani kote. Mara nyingi hadithi ziliwahusu wana wafalme. Mimi nilipendelea zaidi hadithi za vitabu kama zile za Alfu Lela Ulela. Hizi zilikuwa na uhondo mkubwa. Wazazi walizipenda kwa mafunzo yake kwetu sisi. Baada ya kusikiliza hadithi tulizungumza na babu yetu kuhusu yale tuliyoyasikia. Yeye alipenda kutufahamisha kile alichokielewa. Hatukuruhusiwa kubishana naye kwani yeye alikuwa na hekima. Mara nyingi mazungumzo yaliendelea kwa muda mrefu. Ilikuwa raha sana.

F: Lakini kila mtu ana uelewa tofauti. Kwa nini hamkumwambia pale mlipohisi yeye hajaelewa funzo la hadithi?

M: Kuwabishia watu waliozidi umri ni utovu wa adabu mkubwa sana. Tuliruhusiwa kusema labda kuna funzo la nyongeza lakini hatukuthubutu kumbishia Babu yetu. Mvi zake ilikuwa ni alama muhimu ya kuonyesha kwamba amekula chumvi nyingi, yaani yeye ana hekima zaidi yetu.

F: Tuna mengi ya kujifunza kutoka enzi hizo. Ingawa siku hizi kuna vitabu vya kusikiliza. Mtu anaweza kununua na kusikiliza kitabu chote; ni sawa na vipindi vya hadithi au?

M: Ni tofauti kabisa. Zamani tulikuwa na nafasi moja tu ya kusikiliza hadithi, na kama mtu akiikosa ndiyo basi hataipata tena, ingebidi ahadithiwe na wenzake. Pia tulikuwa makini sana kwenye

www.xtrapapers.com



usikilizaji wetu. Hiyo ni tofauti na vitabu vya kusikiliza ambavyo msikilizaji anaweza kurudia rudia anavyotaka.

F: Sikufikiria jambo hilo. Hebu niambie, kila familia ilikuwa na redio ulipokuwa mtoto?

M: Redio hazikuwa bei rahisi. Lakini sote tuliweza kusikiliza vipindi kwani watoto walikwenda kusikiliza redio nyumbani kwa jirani zao ambako walikaribishwa vizuri sana. Mimi binafsi, nilianza kazi nilipokuwa na miaka ishirini na nilipopata mshahara wangu wa kwanza, miaka thelathini iliyopita, kitu cha kwanza nilichofanya ni kujinunulia redio. Redio yangu imewacha kufanya kazi kama miaka mitano iliyopita lakini bado ninayo. Unajua, wakati ule watu walijivunia sana kuwa na redio na baiskeli.

F: Miaka imebadilika sana. Na ulipenda kusikiliza nini kwenye redio yako mwenyewe?

M: Wakati ule nilipenda sana michezo, hasa mpira wa miguu. Basi nikisubiria sana vipindi vya michezo, hasa kuhusu mechi na michuano tofauti. Watangazaji walikuwa hodari sana. Walikuwa na uwezo wa kuelezea yale yaliyotokea uwanjani hadi mtu akahisi kama yeye pia yupo pale uwanjani. Ni kama vile walitupa tiketi za kuingia uwanjani kupitia masikio yetu. Mimi pia nilipenda habari za matokeo ya michezo tofauti, hasa kuhusu timu yangu.

F: Leo umenifunza mengi. Asante sana Steve.

M: Mimi pia nimefurahi kuzungumza na wewe. Hebu niende zangu sasa. Wajukuu wananisubiri.

M: Sawa, nisalimie wote. **

*(Pause 30 seconds.)*

TLR: Sasa sikiliza tena.

*(Repeat from * to **. Pause 30 seconds.)*

TLR: Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 4, na mwisho wa mtihani.

Eng: That is the end of the examination.

Permission to reproduce items where third-party owned material protected by copyright is included has been sought and cleared where possible. Every reasonable effort has been made by the publisher (UCLES) to trace copyright holders, but if any items requiring clearance have unwittingly been included, the publisher will be pleased to make amends at the earliest possible opportunity.

To avoid the issue of disclosure of answer-related information to candidates, all copyright acknowledgements are reproduced online in the Cambridge Assessment International Education Copyright Acknowledgements Booklet. This is produced for each series of examinations and is freely available to download at www.cambridgeinternational.org after the live examination series.

Cambridge Assessment International Education is part of the Cambridge Assessment Group. Cambridge Assessment is the brand name of the University of Cambridge Local Examinations Syndicate (UCLES), which itself is a department of the University of Cambridge.

© UCLES 2021